



KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI TANZANIA
EVANGELICAL LUTHERAN CHURCH IN TANZANIA
REF NO: ELCT/HQ/PD/N023-00031

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) kupitia Idara ya Mipango na Maendeleo, programu ya Maisha Endelevu na Uwezeshaji (ELCT SLEP) inatangaza zabuni ya ununuzi wa chakula kwa ajili wananchi katika vijiji vitatu vilivyoathirika na ukame Halmsahauri ya Urambo Mkoa wa Tabora, KKKT Dayosisi ya Magharibi Kati, Tabora.

Masharti ya waombaji;

1. Awe anafanya biashara katika mkoa wa Dodoma, Tabora na Singida (Ambatisha nyaraka muhimu i.e Lesseni ya Biashara, TIN NK).
2. Awe na uzoefu na uwezo wa usambazaji wa chakula kwa kiasi kinachohitajika.
3. Awe amesajiliwa na mamlaka ya mapato Tanzania na ni mlipa kodi.

S/N.	Aina ya chakula	Maelezo	Kiasi (kg)/litre
1.	Maharage	Soya/maharagwe ya njano	5,700
2.	Mafuta ya kupikia	Alizeti	855
3.	Sukari		1,140
4.	Unga wa lishe	Unga wenye virutubisho kwa ajili ya watoto, wanawake wajawazito na wanaonyonyesha	1,000

Maombi ya zabuni hii yatumwe kwa utaratibu ufuatao;

Waombaji waliopo mkoa wa Tabora waelekeze maombi yao kwa;

**Katibu Mkuu
KKKT Dayosisi ya Magharibi Kati
S.L.P. 782
TABORA
Simu Namba: +255 754 980 419**

Bahasa iliyofungwa kwa lakiri iandikwe juu **“UNUNUZI WA CHAKULA
KKKT DAYOSISI YA MAGHARIBI KATI”** kwa waombaji waliopo mkoa
wa Tabora.

Nyuma ya bahasa iandikwe jina, anwani ya mwombaji na namba za
simu.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 10 Machi 2023 saa kumi kamili
(10:00) jioni.